

**“ULEMAVU BARANI AFRIKA”**

**EPISODE 7: “Kupigania usawa”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 7:**

**MSIMULIZI**

**SCENE ONE: INSIDE THE LIVING ROOM OF THE MALI'S**

- Kangwa (mke, 18)
- Bw. Mali (mume, 50)
- Bl. Mali (mke, 45)

**SCENE TWO : MARKET PLACE IN MAGANYE**

- Oluanda (mume, 18)
- Gidi (mume, 38)
- Wema (mke, 40)
- UMATI ( wake na waume umri tofauti)

**SCENE THREE : AT MAGANYE POLICE STATION**

- Oluanda (mume, 18)
- Gidi (mume, 38)
- Inspekta Joe (mume, 30)

### **UTANGULIZI:**

Salamu nyingi mpenzi msikilizaji wa kipindi hiki cha “Noa bongo,jenga maisha yako”. Sikiliza na uboreshe maisha yako! Hiki nikipindi cha saba tukiangazia, “ **Walemau barani Afrika**”. Ndugu na dada waliosahauliwa katika jamii. Kipindi kilichopita, Oluanda alimweleza Kangwa kuhusu mipango yake, na baadaye, pia akamdokezea mamake, Tofu. Je ni mipango ipi na Oluanda anapanga kuitekeleza vipi? Kangwa, upande mwengine alikuwa tayari kuwaeleza wazazi wake- wakwasi Bw na Bi. Mali – wataukubali usuhuba wake na Oluanda? Tutajua mbivu na mbichi katika kipindi hiki cha leo isimu ya “**Vita vya kutaka haki na usawa**”. Tujiunge na familia ya Mali wanapomsikiliza binti yao Kangwa.

### **SCENE ONE : INSIDE THE LIVING ROOM OF THE MALI'S**

1. **SFX:**                   **MUSIC PLAYS FROM STEREO A BIT LOUDLY**
2. **BW. MALI:**           Kangwa, hebu punguza huo muziki kidogo leo tumekuwa na siku ngumu..  
**VOLUME REDUCED BUT STILL PLAYS FROM BACKGROUND**
3. **BI. MALI:**           Haya, mama. Ulitaka kutuambia nini?
4. **KANGWA:**           Baba na mama. Tangu nikiwa msichana mdogo mulinifunza kuheshimu watu wote, kuwapa usawa na kuwa mnyenyekemu. Sijawahil kufanya hivyo hapo awali lakini sasa nimepata hiyo fursa, na nataka nyinyi munisaidie.

5. **BW. MALI:** Kangwa,Bila shaka, lakini ultaka kufanya nini haswa?
6. **KANGWA:** Nitakueleza baba. Oluanda na mimi tunataka kuhamasisha wale wote walio na ulemau wowote wa kimaumbile hapa Maganye, na tupange maandamano ya amani... itatulazimu....
7. **BI. MALI:** **(Shocked)** Ati? Hebu rudia tena?
8. **BW. MALI:** Mama Kangwa, hebu muache mwanetu amalize usemi wake kwanza...
9. **KANGWA:** Asante baba, mnafahamu yaliyompata Oluanda. Alifukuzwa shule ati sababu yeye ni mlemau. Watu hawa hawapewi nafasi sawa kamwe. Lakini unajua nini? Hata wao wana ndoto na maono. Mbali na hayo,sisi, watu tunaojiita kamili huzidi kuwagandamiza. Katika sehemu za umma ni ngazi pekee zinazojengwa, bila kujali wanaotumia magongo na vigari vya walemau. Katika mashule wanahujumiwa, madukani hawathaminiwi, licha ya kuwa hawaajiriwi kazi. Ungelihisi nini kama ingelikuwa wewe? Ungelihisi nini kama ingelikuwa ni mimi? Tutawalaumu kweli watakapo ombo?

10. **BW. MALI :** (**Impressed**) Hapana! Binti yangu. Huo ni mtazamo mzuri. Niko tayari kukusaidia kwa hali na mali. Nafurahi mno kuwa nina binti kama wewe.
11. **BI. MALI:** (**Hysterical**) Nyinyi wawili mumepagawa? (**Shocked**) mumewangu, umeelewa maneno anayosema Kangwa kweli?
12. **BW. MALI:** (**Happy mood**) Bila shaka. Binti yetu anataka kuwasaidia wale ambao miaka mingi wamekuwa wakigandamizwa humu kijijini. Hajawahi kuzungumza mambo ya busara kama haya awali.
13. **BI. MALI :** Kangwa, binti mrembo wa Bw na Bi. Mali, akiandamana mavumbini Maganye amezungukwa na vilema, vipofu, mabubu kutoka kila pahala. Hiyo picha iko sawa kwako?
14. **BW. MALI:** Tena sawa kabisa. Isitoshe, hata kuwa pekee. Nitakuwa nae ubavu kwa ubavu!
15. **KANGWA:** Asante baba. Mama pia wewe utajiunga nasi? Nataka tuchukuwe jukumu kama familia..
16. **BI. MALI:** (**Dry sarcasm**) Hata nikauwawa! Kama nyinyi wawili mwataka kujigiza kuwa mama Theresa na Nelson Mandela. Karibuni. Naenda kulala .

17. **SFX:** **HIGH HEEL SHOES WALK AND FADE AWAY**
18. **BW.MALI:** Usijali kuhusu mamako. Ameudhiwa na mambo mengine. Najua hasira zikimwisha atabadili mawazo yake . Nieleze zaidi kuhusu huyu kijana....
19. **MSIMULIZI:** Kangwa alimuhadithia babake yote anayojuwa kumhusu Oluanda, na Bw. Mali akavutiwa, alitaka sana kukutana na Oluanda. Siku iliyofuata, badala ya kupiga rangi na kushona viatu, Oluanda alijiandaa kutoka nyumbani. Aliamuwa kuzuru soko la Maganye ili kuwanasihi walemovu wengine mule sokoni, waliokwenda kuombaomba wanunuzi na watembezi wengine. Miongoni mwa walemovu hao walikuwa Gidi na Wema. Endelea kusikiliza.

## **SCENE TWO: MARKET PLACE IN MAGANYE**

20. **SFX :** **MARKET AMBIENCE**
21. **WEMA:** **(Begging, sound of some coins)** Saidia.. saidia maskini niko na watoto wawili.. tafadhali saidia..
22. **OLUANDA:** **(Calling out)** Sikilizeni. Tafadhali naomba munisikize. Kwa majina naitwa Oluandana nina jambo muhimu la kuwaeleza. Wengi wenu hamunijui,hilo sio muhimu kwa sasa. Niko hapa kwa ajili ya matatizo hayo yanayowakumba kwa sababu pia mimi yananikumba. Ni miaka mingi

jamii imekuwa ikitutenga. Hili, lazima likome!

23. **SFX:** **CROWD MURMURS IN DISAGREEMENT/ AGREEMENT**
24. **OLUANDA:** Ninapowatazama mukiombaomba sioni sababu muafaka ya kufanya hivyo kwani wengi wenu, muna uwezo wa kukikuza kijiji chetu mutakapopewa nafasi hiyo. Na kama ilivyo, kwa sasa hawataki kutupa nafasi hiyo basi ipo haja ya kupigania nafasi hiyo!!!,
25. **WEMA:** Huyu kijana anatupotezea wakati. Anajuwa nini? Hajui sisi tuna familia za kulea?
26. **OLUANDA:** Kweli, sina familia ya kulea na pia mimi ni mdogo ki umri kati yenu hapa. Lakini hilo halibadilishi ukweli wa kuwa sote tumenyimwa haki zetu. Nilipokatwa mguu wangu mimi nilifukuzwa shule. Sijui hadithi zenu lakini lazima kuna pahala umewahi kutengwa au kunyimwa haki yako kwa sababu wewe ni mlemavu!
27. **GIDI:** Kijana anasema ukweli. Nilipoteza kazi yangu kiwandani baada ya kupata ajali na kupoteza jicho moja. Baada ya hapo sikuweza tena kupata kazi nyengine, nimezuru warsha nyingi za walemavu. Munajua kuwa asilimia 80 ya walemavu waliofikia umri wa kufanya kazi

amba hawaajiriwi!

28. **SFX:** **MORE MURMURS FROM CROWD**
29. **OLUANDA:** (**Shocked**) Ati asilimia 80? Na sina shaka hao asilimia 20 ambao wameajiriwa wanalipwa mshahara duni au wamejajiri wenyewe!
30. **WEMA:** Kijana, chunga mdomo wako! Sasa unatushauri tufanye nini?
31. **OLUANDA:** Wengi wenu munapiga kura msimu huo unapofika sivyo?
32. **GIDI:** Kulingana na hesabu , walemvu wanatimia asilimia10 ya jumla ya hesabu ya watu nchini.
33. **WEMA:** Zungumza lugha rahisi tuelewane! Ukitaja maasilimia si wote tulienda shule eti, ala!
34. **GIDI:** Samahani, umesema kweli. Ni asilimia 1 pekee ya wanawake walemvu katika nchi zilizoendelea ndio wamesoma. Yani wanaweza kuandika na kusoma.
35. **OLUANDA:** Sawa, ni hivi. Tuseme hapa Maganye kuna wakaazi 500,000, asilimia10 yake watakuwa...
36. **GIDI:** 50,000. Watu eh, sio pesa...  
**(Laughter from crowd)**

37. **WEMA:** Haiwezekani! Kwani tuko wengi sana hapa  
Maganye?wengine wako wapi? Tunaojijuwa ni  
wachache tu...
38. **OLUANDA:** Swali zuri. Lakini jibu tunalo. Wengine wetu  
wamefichwa; hata labda ni kwa sababu ya hila  
za familia zao. Lengo langu ni kuwaauliza  
wanasiasa, serikali, viongozi wa kidini na  
wowote wale wajue kuwa sisi tuko na matatizo  
yetu ni kadha wa kadha. Kutekeleza hayo ni  
sharti tuwe na maandamano ya amani...
39. **SFX:** **MURMURS AND LAUGHTER FROM CROWD**
40. **OLUANDA:** Labda hamuoni umuhimu wake, lakini  
tutawakilisha hoja zetu! tutasikika. Hatufai  
kudharauliwa na mwanasiasa yejote iwapo  
tunazo kura 50,000.
41. **GIDI:** Oluanda, sitaki kukuvunja moyo lakini hili  
sidhani kama litawezekana. Maneno ni matamu  
sana. Lakini je tutakapotumiwa vikosi vya  
askari? Umefikiria hilo?
42. **OLUANDA:** La, sijafikiria hilo. Lakini ni nani atakayemtupia  
mlemavu bomu la kutoa machozi? Jamii  
haitakubali hayo pia! Ama?
43. **GIDI:** Labda unasema kweli. Tuombe iwe vile

usemavyo.

44. **MSIMULIZI:** Oluanda aliwashawishi walemau fulani kijiunga nae katika maandamano jijini ili kushinikiza haki zao. Baada ya hapo alihitaji kuzungumza na marafiki zake wa kitambo, Magoto na Karem. Pia walihitaji kibali cha maandamano kutoka kituo cha polisi cha Maganye. Hivyo, Oluanda na Gidi walikwenda kituo kilichokuwa karibu na soko na inspeka Joe alikuwa yuko kwenye zamu.

### **SCENE THREE: AT MAGANYE POLICE STATION**

45.      **SFX:**      **OLD TYPEWRITER BEING USED TO TYPE;  
OFFICE TALK IN THE BACKGROUND;  
POLICE CAR SIRENE FROM OUTSIDE**
46.      **GIDI:**      Habari afisaa.
47.      **SFX:**      **TYPING CONTINUES,SOUND OF  
CRUTCHES APPROACHING**
48.      **OLUANDA:** **(Calmly)** Samahani bwana, tunaweza...
49.      **INSP.JOE:** **(Irritated)** Muna nini nyinyi watu? Hamuoni niko kazini? Haya shikeni!
50.      **SFX:**      **COINS JINGLING IN POCKET, THEN PUT ON  
TABLE**
51.      **INSP. JOE:** Hizi ndizo niko nazo leo... ondokeni!

52. **GIDI:** Bwana, hatukujia senti zako. Tumekuja hapa kuuliza kibali.
53. **INSP.JOE:** (**Surprised**) Kibali? Kibali gani? Kwani munahitaji kibali kuombaomba hapa? Sijaona hiyo!. (**regret**) Poleni sio ati ninasema kuwaudhi nyinyi. Singependa kuwa katika hali yenu. Poleni tena. Sasa kibali ni cha nini?
54. **OLUANDA:** Sisi ni wawakilishi wa walemvu hapa Maganye. Tunaomba kibali cha kufanya maandamano ya amani...
55. **INSP.JOE:** (**Laughs out loud**) Munataka kunivunja mbavu. Hicho ni kichekesho kizuri sana lakini sasa nina kazi zakufanya (**Pause**) Hivi kumbe si mzaha? Alaa, sawa, malalamishi yenu ni nini?
56. **GIDI:** Kiburi kama chako. Watu hawatuchukulii kama wanadamu mara nyingi. Tunahitaji nafasi sawa katika jamii..
57. **OLUANDA:** Ndio tuko hapa kuuliza kibali na ulinzi wakati huo wa maandamano
58. **INSP.JOE:** (**Serious tone**) Sasa jambo kama hili ni geni kwangu, siwezi kuamuwa peke yangu. Itanibidi niongee na wakubwa. Tafadhali rudini kesho.

**HITIMISHO:**

Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Oluanda na Gidi hawangeweza kumshurutisha Inspeksa Joe zaidi. Waliondoka kurudi sokoni kuwa taarifu wenzao waliowangoja pale. Kutatokea nini baadaye? Je, askari watawaruhusu? Je, waliokuwa nae shuleni Oluanda watasema nini baada ya kualikwa na Kangwa .Je, wanasiasa watamuelewa na kumuunga mkono? Usikose majibu hayo na mengineo katika kipindi kifuatacho. Ukitaka kusikiza tena kipindi hiki au chengine tafadhali tembela tovuti zetu [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe).

Hadi wakati huo,nakutakia wakati mufti.